# ‘’SHERIA MPYA NI MWAROBAINI WA KUKOSEKANA KWA TAKWIMU SAHIHI ZA MATUKIO YA VIZAZI VIFO NDOA NA TALAKA ’’

Serikali imeanza maboresho ya mfumo wa usajili kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu unaojulikana kama (CRVS) ambao unalenga kutatua changamoto ya idadi ndogo ya usajili wa matukio ya vizazi,vifo na sababu zake, ndoa na talaka na kusababisha Taifa kukosa takwimu sahihi kwa ajili ya mipango mbalimbali ya maendeleo.

Hayo yamesemwa na Warizi wa Katiba na Sheria Prof Palamagamba Kabudi wakati akizungumza na Wahariri wa vyombo vya habari hii leo Mkoani Morogoro kwenye semina ya kuwajengea uwezo na ufahamu kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na takwimu kwa kufanya marekebisho ya Mfumo wa Sheria zinazosimamia masuala ya usajili wa matukio hayo muhimu na kuahidi kukamilisha kazi hiyo mwishoni mwa mwaka huu.

Aidha Prof Kabudi ameongeza kuwa Usajili wa matukio muhimu ndio mfumo mama katika nchi yoyote kwani ndiyo unaosajili taarifa za mtu anapoingia duniani kwa kuzaliwa, unaweka kumbukumbu kadiri anavyokuwa na kupita katika hatua mbalimbali mpaka anapotoka duniani kwa kufariki na taarifa za kwenye mfumo huu hupaswa kutumika na mifumo mingine ya Serikali kama kianzio (input) kwa mifumo mingine ya Serikali kama ya uraia, utaifa na daftari la wapiga kura.
‘’Taarifa za matukio hayo zitaisaidia Serikali na wadau wengine hasa wa sekta ya afya kupanga mipango ya afya ya jamii pamoja na kulinda rasilimali muhimu za Taifa na kwa hivi sasa kukuza uchumi kupitia viwanda kwa kuwa na takwimu sahihi za makundi yote ya wananchi kutokana na ukweli kwamba zitawawezesha wawekezaji kujua uhakika wa masoko ya bidhaa zao na nguvu kazi iliyopo kwa ajili ya kupata wafanyakazi katika sekta hiyo’’.amesema Prof Kabudi

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya ushauri ya RITA Prof Hamis Dihenga amesema Changamoto zinazosababisha hali isiyoridhisha ya usajili ni pamoja na mfumo na sheria uliopitwa na wakati, taratibu za usajili zisizo rafiki, gharama za nyaraka zinazinaokana mfumo huo, umbali wa vituo ya usajili, kukosekana utangamano na mifumo mingine pamoja na uelewa mdogo wa umuhimu wa usajili na kwa sasa Wakala umeshaanza kuchukuwa hatua kwa  kutekeleza Mpango wa usajili wa Watoto wenye Umri

chini ya miaka mitano ambao wanasajiliwa katika ofisi za kata na vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya Mama na Mtoto.

Prof Dihenga ameongeza kuwa tayari takribani mikoa saba (7) ya Tanzania Bara ambayo ni Songwe,Mbeya, Mwanza, Iringa,Njombe, Shinyanga na Geita inaendelea kutekeleza mpango huo na kati ya hiyo Mikoa minne imefanikiwa kwa kusajili Watoto wote wa umri huo kwa asilimia mia moja.

Naye Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA Emmy Hudson amebainisha kuwa, wakati mifumo ya sheria ikiendelea kufanyiwa maboresho tayari kwa upande wa teknolojia na upatikanaji wa huduma umeanza kuimarika katika ofisi za RITA Makao Makuu na zile zilizopo kwa Wakuu wa Wilaya kote nchini kwa kuanza na upande wa malipo ya ada mbalimbali za huduma kwa njia ya kielekroniki na kufunga mfumo wa TEHAMA katika uandaaji na uchapati wa vyeti na hivyo kuongeza kasi ya usajili wa vizazi,vifo ndoa na talaka ndani ya muda mfupi ikilinganishwa na hapo awali.

Wakati huohuo Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Theophil Makunga amesema kupitia semina hiyo wameweza kufahamu kwa undani shughuli mbalimbali zinazofanywa na RITA na kubainisha kuwa hapo awali walikuwa wakichanganya majukumu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na idara ya uhamiaji kwa kuamini Mtu akiwa na cheti cha kuzaliwa tayari amekuwa raia wa Tanzania kumbe zana hiyo si ya kweli, na kutoa wito kwa wanahabari kwa ujumla kushirikiana na Wakala kwa kuandika habari zenye takwimu sahihi ili kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu ambayo ni vizazi,vifo,ndoa na talaka.

‘’Katika vyombo mbalimbali vya habari kumekuwa na mkanganyiko wa kutokutumia kiswahili sanifu pamoja na kuchanganya kazi za taasisi ya RITA na Nida, mara nyingine waandishi wameiita RITA kama mamlaka ya kutoa vyeti vya kuzaliwa wakati sio mamlaka bali ni Wakala’’ amesema Makunga.

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini(RITA)umeweka utaratibu kila mwaka kukutana na wadau wake wa sekta ya habari ambapo kwa mwaka huu Jukwaa la Wahariri wamepatiwa semina ya siku moja Mkoani Morogoro kuhusu Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu unaojulikana kama (Civil Registration and Vital Statistics - CRVS) na kisha baadaye kupata fursa ya kusajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa pamoja na familia zao kupitia dawati maalum la usajili lililofunguliwa mahsusi kwa ajili yao.